TANGAZO LA SERIKALI NA. 278 tarehe 7/4/2023

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 9(1) na (2))*

HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA (MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI MUSOMA) (KUONGEZA ENEO LA KUTOA HUDUMA)(MAREKEBISHO) NOTISI YA MWAKA 2023

Jina

TS. Na. 353 la mwaka 2022

1. Notisi hii itajulikana kama Huduma za Maji na Usafi na Mazingira (Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Musoma) (Kuongeza Eneo la Kutoa Huduma) (Marekebisho) Notisi ya Mwaka 2023 na itasomwa kwa pamoja na Notisi ya Huduma za Maji na Usafi na Mazingira (Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Musoma) (Kuongeza Eneo la Kutoa Huduma) ya Mwaka 2022 ambayo katika Notisi hii itarejewa "Notisi Kuu".

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

2. Jedwali la Kwanza la Notisi Kuu linarekebishwa kwa kufuta maneno "Bunda Town".

Marekebisho ya Jedwali la Pili

3. Jedwali la Pili la Notisi Kuu linarekebishwa kwa kufuta maneno "Bunda Water Supply and Sanitation Authority".

Dodoma,
8 Machi, 2023

JUMAA H. AWESO
*Waziri wa Maji*